


ILANI YA

# UCHAGUZI MKUU 2020

**Mpendwa Mtanzania mwenzangu**

Nakukaribisha katika safari mpya tuliyoanzisha. Tunaelekea katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Pengine una maswali unajiuliza, tumekusudia kufanya nini? Tutajenga Tanzania yenye watu wenye hali bora kijamii na furaha ya kweli, yenye kujali utu, yenye mfumo mzuri wa utoaji haki, yenye demokrasia ya kweli, yenye uhuru na yenye uchumi jumuishi, imara na unaostawi.

Tanzania ambayo kila mtanzania; mtoto, kijana, mwanamke, mwanamume, mzee, wa kijijini na mjini ana haki sawa mbele ya sheria na ana fursa stahiki za kujenga na kujifikia ndoto zake. Tanzania ambayo, watanzania wanajivunia kuwa watanzania na sio Tanzania hii ya sasa ambayo mamilioni ya watanzania wanavumilia kuwa watanzania.

Uchumi wa taifa utakuwa uchumi jumuishi, wa watu na si wa vitu. Uchumi wa Wananchi wengi na si uchumi wa Serikali na kundi la wachache. Serikali yetu itawekeza kwenye sekta zinazoajiri Watanzania wengi, hasa Kilimo, Ufugaji na uvuvi, pia itaboresha na kuwezesha ustawi wa sekta isiyo rasmi hasa ya biashara ndogondogo. Mifumo ya kodi na urasimishaji biashara vitalenga katika kuleta ufanisi na kukuza biashara na si kudumaza na kuleta ukiritimba.

Yako mambo mengi tumekusudia kufanya ili kuboresha maisha yetu. Ndio maana tunasema itakua awamu ya #KaziNaBata. Yaani kila Mtanzania afaidi jasho lake na aone fahari kuwa sehemu ya Taifa hili.

Karibu ujisomee Ilani yetu, kisha fanya maamuzi sahihi.

Wasalaam,

**Zitto Zuberi Kabwe,**
Kiongozi wa Chama



# MAMBO GANI TUMEMPITIA MIAKA 5 ILIYOPITA?

Katika miaka mitano iliyopita (2015-2020), nchi yetu imepitia na inaendelea kupitia misukosuko mingi mikubwa iliyosababishwa na utawala wa kikandamizaji wa Chama Tawala. Makundi mbalimbali, kama si yote, ya jamii yetu yameumizwa na maamuzi, sera na matendo ya watawala wa nchi yetu.

## *Kodi kubwa zinazofukarisha wananchi*




## *Waandishi na Wanaharakati kuumizwa*



## Wafanyabiashara kufilisiwa




## Mwingiliano wa Mihimili ya Nchi



## TUKICHAGULIWA TUFANYANYA NINI?



Tutaruhusu Uhuru zaidi kwa kila Mtanzania kwani ni haki yao msingi.

**a). Tutafanya nini kuhusu Uhuru wa kutoa maoni?**

Ndani ya siku 100 za kwanza tangu kuingia madarakani, Serikali ya ACT Wazalendo itafuta Sheria zote zinazobana, kuminya na kufifisha haki na uhuru wa Watanzania kujieleza na kutoa maoni.




**b). Uhuru wa vyombo vya Habari je?**

Serikali ya ACT Wazalendo, ndani ya miezi sita (6) ya kwanza itafanya yafuatayo;

- Itafuta sheria zote kandamizi na zinazopora uhuru wa vyombo vya habari, na kutengeneza sheria, kwa kushirikiana na wadau, zitakazolenga kuleta uhuru na weledi na ukuaji wa sekta ya habari.
- Itahakikisha vyombo binafsi vya habari vinakuwa na haki sawa ya kupatiwa taarifa na kuripoti habari na matangazo ya biashara kutoka Serikalini.

- Itahakikisha vyombo vya habari vya umma vinakuwa huru kutoa taarifa yoyote kwa maslahi ya umma bila kuingiliwa au kushawishiwa na chama kilicho madarakani.




- Itaunda Tume maalum kutoa kuratibu na kusimamia ajira kwenye sekta ya habari na sanaa. Kila mwandishi wa habari atakuwa na mkataba wa ajira na waajiri watalazimika kuhakikisha kila mwandishi anapatiwa Hifadhi ya Jamii na Bima ya Afya.

**c). Uhuru wa Kukusanyika je?**

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itasimiamia uhuru na haki ya mtu mmoja mmoja, Asasi za Kiraia, Jumuiya za kijamii na Kitaaluma, pamoja na makundi mbalimbali ya jamii kukutana, kuungana, kushirikiana na kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na miongozo yao bila kuvunja Katiba ya nchi.

- Itafanyia marekebisho sheria kandamizi inayotoa mwanya wa wazi kwa Polisi kuzuia uhuru wa kujumuika bila sababu yoyote ya msingi, hivyo kukengeuka Katiba yetu ya nchi ya 1977 ibara ya 20 (1) inayoruhusu Uhuru wa Kukusanyika.

**Kuhusu Usawa je?**

Chama cha ACT Wazalendo, kinaahidi kuijenga Tanzania inayotumia rasilimali za nchi kwa usawa bila ubaguzi wa kikabila, kikanda, kimkoa kiitikadi, kidini wala kisiasa.

**a). Usawa mbele ya sheria**

Serikali ya ACT Wazalendo itahakikisha kila Mtanzania ana haki na wajibu sawa mbele ya sheria bila kujali cheo, jinsia, hali, dini, kabila wala itikadi ya siasa. Shabaha ni kuwa Taifa la Tanzania lenye haki na usawa kwa kila raia.



**b). Usawa wa Kijinsia:**

Ili kuleta usawa wa kweli wa kijinsia, Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itahakikisha ushiriki wa 50 kwa 50 katika ngazi zote za uongozi, hasa kwenye nafasi za kuteuliwa.
- Itarekebisha sheria za mifumo ya uwakilishi wa wanawake hasa bungeni (Viti maalumu), ili kuleta mfumo utakaokuza na kuboresha ushiriki wa wanawake katika Bunge hasa kutoka kwenye majimbo.
- Itawekeza katika mifumo itakayowezesha wanawake kuwa wafanyabiashara wakubwa, na wamiliki wa mifumo ya uzalishaji mali na ajira, ili kuondokana na dhana kuwa wanawake ni watu wakufanya shughuli ndogo ndogo za uchumi.
- Itaondoa kodi na kuwezesha upatikanaji bure wa bidhaa za hedhi katika shule za msingi na sekondari Tanzania nzima.
- Itakomesha ukeketaji wa wanawake na watoto wa kike. Aidha, Serikali yetu itahakikisha utekaji unamalizika ndani ya miaka 10, kama ambavyo mpango wa malengo endelevu ya dunia unavyoelekeza.
- Itadhibiti mimba za utotoni kwa kuhakikisha watoto wote wa kike wanapata elimu katika mazingira salama na kuhakikisha elimu rika inatolewa kwa ubora katika taasisi zote za elimu nchini ili kuwajengea uwezo watoto wa kike na wa kiume kuepuka na kutoa taarifa za unyanyasaji wa kingono.
- Itatoa elimu sahihi na huduma rafiki za afya ya uzazi kwa vijana, hasa wa kike walioko shuleni na nje ya shule, kwa kushirikiana na asasi za kiraia na Taasisi za Afya.

- Itahakikisha utekelezaji wa sheria zinazolinda watoto dhidi ya ubakwaji pamoja na unyanyaswaji wa kingono kwa ujumla. Serikali yetu itaweka hadharani 'orodha ya waliotiwa hatiani kwa kubaka na kunyanyasa kingono wanawake na watoto'.




- Itasimamia uwepo wa usawa katika malezi ya watoto, hasa baada ya wazazi kutengena au pale watoto wanapozaliwa nje ya ndoa.
- Itakomesha ukatili dhidi ya wanawake na watoto, hasa ukatili wa kingono, kimwili na udhalilishaji kwenye mitandao.

**Tutafanya nini kuhusu usimamizi na utoaji wa Haki?**

Serikali ya ACT Wazalendo itatekeleza kwa vitendo Sheria, Kanuni na Mikataba yote ya kimataifa inayolinda na kuhifadhi haki za binadamu.

**a). Haki ya kupata habari:**

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo ili kuhakikisha uwepo wa haki ya kupata habari;

- Itaboresha ushiriki wa Tanzania katika mpango wa Afrika kujitathmini kiutawala bora (APRM).

- Itairudisha Tanzania katika uanachama Mpango wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP), ili kuhakikisha Serikali inaendeshwa kwa uwazi mkubwa na kila Mtanzania anapatiwa haki yake ya kupata habari sahihi kwa wakati sahihi.
- Itarudisha matangazo ya moja kwa moja ya Bunge (bunge live) – na kuwa na idhaa ya mtandaoni ya Bunge, ili kuhakikisha wabunge wanapata nafasi ya kutosha kufafanua hoja zao kwa kina hata nje ya vikao vya Bunge.




- Itafanyia marekebisho makubwa ya Sheria ili kuhakikisha mikataba yote ya miradi yenye maslahi mapana ya Taifa, kama madini, kandarasi, miradi ya ujenzi itawekwa wazi.

**b). Haki ya kushiriki katika kufanya maamuzi je?**

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;


- Itashirikisha kikamilifu wananchi kwenye kufanya maamuzi ya kila jambo ambalo lina maslahi mapana kwa Taifa, aidha kwa kupigia kura moja kwa moja, au kutoa maoni yao kwa njia ya maandishi (petition), au kupitia wawakilishi wao wa majimbo.

- Itaweka kisheria utaratibu wa wananchi wanaoishi kwenye maeneo yenye rasilimali kutoa idhini ya miradi ya uvunaji wa rasilimali hizo kuanza kutekelezwa.

### c). Tutalindaje Haki za watu wenye ulemavu?

Serikali ya ACT Wazalendo, itaweka kipaumbele katika kuhakikisha haki za watu wenye ulemavu zinalindwa, kuhifadhiwa na kuhamasishwa kwa kufanya yafuatayo;

- Itaweka taarifa zote muhimu za umma kwenye mifumo sahihi na wezeshi kwa watu wenye ulemavu, kwa mfano, kutafsiriwa kwa lugha ya alama na nukta nundu.
- Itasimamia utekelezaji wa sheria ya majengo ili kuhakikisha majengo yote ya umma yanafikika kwa urahisi kwa watu wenye ulemavu.
- Itahakikisha upatikanaji wa uwakilishi wa haki na wenye tija wa watu wenye ulemavu katika uongozi, ngazi za maamuzi na shughuli za kuingiza kipato.
- Itahakikisha wasichana na wanawake wenye ulemavu wa viungo na wanaoishi kwenye mazingira magumu wanapatiwa bidhaa za hedhi bure.
- Itahakikisha kaya maskini na zinazosimamiwana wanawake na kulea watoto wenye ulemavu watapatiwa pesa za kujikimu kila mwezi kutoka kwenye mfuko maalumu wa 'kuwezesha watu wenye ulemavu'.
- Itahakikisha watu wenye ulemavu wote nchini wanapata fursa sawa za kujifunza na kupata ajira stahiki katika fani na sekta mbalimbali, hii ni pamoja na kuwekeza kwenye vifaa maalumu na vya kisasa vya kujifunzia kwenye shule maalum za watu wenye ulemavu.



**Namna gani tutasimamia Utawala wa Sheria?**

Hakuna na hakutakuwa na aliye juu ya sheria kwenye Serikali itakayoongozwa na ACT wazalendo. Kila kitu katika Serikali yetu kitaongozwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizoanishwa na vyombo mahususi vyenye mamlaka hiyo.

**a). Tutafufua mchakato wa Katiba Mpya**

Serikali ya ACT Wazalendo ndani ya miaka miwili itafufua na kukamilisha mchakato wa kutengeneza Katiba Mpya kwa kuwashirikisha Watanzania kikamilifu. Katiba hii mpya;

- Itaboresha Muundo wa Muungano ili kuwa na Muungano wa Usawa, wa Haki na wenye Kuheshimiana, na kusimamia uundwaji wa muundo wa Serikali tatu.
- Itaainisha na kuimarisha misingi ya haki na usawa kisheria, na kuweka nyenzo madhubuti za kusimamia haki, usawa, na uhuru kwa raia wake.

- Itajali maslahi mapana ya Taifa letu na kuimarisha uwajibikaji.
- Itasimamia uwepo wa 'Serikali ya Umoja wa Kitaifa' badala ya kulimbikiza viongozi wa chama kimoja.
- Italeta mfumo bora wa kuendesha Serikali hasa za mitaa – kwa kuwezesha ugatuaji (madaraka zaidi kwa Serikali za Mitaa badala ya Serikali Kuu).
- Itawapa wananchi haki ya kuchagua wakuu wa mikoa kuanzia uchaguzi mkuu wa mwaka 2025
- Itaimarisha uhuru na uimara wa mihimili yote ya Serikali.



- Itatoa haki kwa Watanzania kuwa na Uraia Pacha.
- Itatengeneza dira ya Tanzania ya miaka mia moja inayokuja.

**b). Kuimarisha Uwajibikaji**

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itaimarisha taasisi za kusimamia uwajibikaji kama Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAOT), Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) kwa kuhakikisha mchakato wa uteuzi wa wakuu wa Taasisi hizo unaidhinishwa na Bunge baada ya uteuzi wa Rais.
- Itahakikisha uhuru wa taasisi za kusimamia uwajibikaji nchini.
- Itahakikisha haiwavumilii viongozi wote ambao ni kikwazo kwa uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi.
- Itasisitiza uwazi wa taarifa kwenye mikataba yote mikubwa ili kuwezesha taasisi zinazosimamia uwajibikaji nchini zinapata urahisi katika kazi yake.

**c). Kupambana na rushwa na ufisadi**

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itatoa elimu kwa umma kuhusu rushwa na namna wananchi wanavyoweza kushiriki kwa pamoja kutokomeza rushwa kubwa (ufisadi) na ndogo.
- Kwa kushirikiana na mataifa ya jirani na rafiki, itaandaa orodha ya makampuni na taasisi zinatoa rushwa kupata miradi, ili kuondoa mianya ya rushwa katika manunuzi hasa ya nje.
- Kudumisha uwazi katika utendaji wote wa Serikali kwa kurekebisha sheria ya watoa taarifa (Whistle blowers act), ili kutoa kinga na ulinzi kwa watakaofanya kazi hii ya kizalendo ya kutoa taarifa.

### d). Kulinda maadili ya kazi

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo ili kulinda maadili ya kazi;

- Itabadilisha kabisa mfumo na utendaji wa Tume ya Maadili ya Umma ili kuipa nguvu na nyenzo za kusimamia kikamilifu maadili ya utumishi wa umma, kwa kuweka utaratibu wa kisheria utakaoelekeza uteuzi wa Viongozi wa Tume hii kufanywa na Tume ya Kijaji, chini ya Jaji Mkuu na kufanyiwa usaili na kuthibitishwa na Bunge/Kamati ya Bunge ili kuhakikisha wanawajibika kwa wananchi na siyo kwa viongozi wachache wanaowateua.
- Itaboresha muundo na utendaji wa vyombo vya dola ili kuviwezesha kufanya kazi zake kwa uhuru bila kuingiliwa kisiasa na kutekeleza majukumu yake kwa kufuata sheria na Katiba.



## JINSI GANI TUTALETA UFANISI NA UBORA WA HUDUMA ZA JAMII?

**a). Kwa kuboresha Elimu:**

Serikali ya ACT Wazalendo, itatoa elimu bila malipo (bure) katika shule za awali, msingi, sekondari, vyuo vya ualimu, vyuo vya ufundi (VETA) na vyuo vya utabibu.

**Tutafanya nini katika Elimu ya Msingi?**

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itaongeza vyumba vya madarasa 24,000 kila mwaka ili kutosheleza ongezeko kubwa la watoto mashuleni.
- Itapanua uwezo wa vyuo vya walimu kudahili ili kuzalisha walimu 20,000 kila mwaka ili kukidhi hitaji la ongezeko la wanafunzi.
- Itafanyia mabadiliko makubwa mtaala wa shule ya msingi na sekondari ili kuhakisha elimu ya msingi inamtengenezea kila mwanafunzi msingi mzuri wa maisha yake, mfano, kuwa na masomo mahususi kama kujitegemea, ubunifu na upembuzi, ili kujenga ufahamu na uelewa wa mambo ya msingi katika kukabiliana na kubadilisha mazingira ya jamii zao.
- Itahakikisha vitabu na zana nyingine za kufundishia na kujifunzia vinatolewa bure kwa kila shule za serikali kwa ubora na wakati sahihi.
- Itahakikisha haki na stahiki za walimu ni kipaumbele. Tunaamini, bila walimu wenye maslahi bora, mazingira mazuri ya kuishi na kufanyia kazi, na fursa za kuongeza taalamu na kupanda madaraja kwa wakati, ari ya kufanya kazi hupungua, na hivyo kudumaza utoaji wa elimu.

## Tutaboreshaje Elimu ya Sekondari?

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itaboresha ufundishaji, ujifunzaji na ubunifu hasa katika masomo ya sayansi na teknolojia. Hii itakuwa ni pamoja na kuhakikisha kila shule ya sekondari Tanzania ina maabara na maktaba.




- Itaajiri wafanyakazi wasio walimu, kama wana maabara, wakutubi, na walezi ili kuhakikisha ubora wa upatikaji wa elimu na ubora wa malezi ya wanafunzi wakiwa shuleni.
- Itajenga mabweni yenye huduma zote stahiki hasa kwa watoto wa kike kudhibiti utoro, mdondoko na mimba za utotoni.

## Elimu ya Ufundi je?

Serikali ya ACT Wazalendo, itahakikisha;

- Inawekeza katika elimu iliyojikita katika uvumbuzi wenye kuleta suluhu ya changamoto za kila siku za maisha ya mtanzania, wa kawaida. Tumedhamiria kufanya vyuo vya ufundi siyo tu viwe vyuo vya kujifunza kurekebisha vitu mbalimbali na kusoma historia ya uvumbuzi, bali viwe vyuo vinavyojikita katika kuvumbua na kutengeneza.

- Itahakikisha kuwa Mitaala ya vyuo vya ufundi inabadilishwa ili kutengeneza mitaala inayotoa mafunzo yanayoakisi mahitaji ya soko la dunia,




- Kuwa katika Kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji) kunakuwa na angalau Chuo kimoja cha Mafunzo ya Ufundi (VETA),
- Inaweka mfumo utakaomuwezesha mhitimu wa chuo cha VETA kuweza kujiendeza zaidi kielimu na kujiunga na mifumo mingine ya elimu.
- Kutakuwa na vyuo vya Ufundi Mchundo vyenye uwezo wa kudahili wanafunzi wasiopungua 10,000, angalau katika nusu ya Mikoa ya Tanzania Bara.
- Ada ya Masomo , Fedha za Vitabu (Stationeries), na gharama za Mafunzo kwa Vitendo (Field Studies/Internship) kwa kila mwanafunzi anayedahiliwa katika chuo cha Elimu ya Chuo cha Ufundi Mchundo itagharamiwa na Serikali.

**Vipi kuhusu Elimu ya Juu?**

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itatoa ruzuku ya sawa na asilimia 40% ya bajeti ya chuo kwa vyuo vikuu kufanya tafiti mbalimbali zitakazotoa dira na miongozo kwenye fani mbalimbali hasa za sayansi ya jamii ili kuwa na Serikali na jamii inayofanya maamuzi ya kitaalamu.
- Itawekeza kwenye mifumo ya kisasa itakayoongeza ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji katika vyuo vikuu, na kuwapunguzia wahidhiri mzigo mkubwa katika kutoa mihadhara.
- Itaajiri wahadhiri wasiopungua 5,000 kwa miaka mitano ili kupunguza uwiano mkubwa uliopo kati ya wahadhiri na wanafunzi.
- Itaboresha mazingira mazuri ya vyuo hasa ujenzi wa vyoo na mifumo ya maji safi na majitaka.
- Itadhibiti ubora wa vyuo vikuu binafsi ili kuhakikisha kila chuo kinaandaa wahitimu walio bora na wenye weledi wa hali ya juu.
- Itaanzisha vyuo vikuu vya Taifa vipya vitano vyenye uwezo wa kudahili wanafunzi wasiopungua 20,000 kila kimoja, vitatu Tanzania Bara (Mtwara, Kigoma na Tanga), viwili Zanzibar (Pemba na Unguja).
- Itafuta mikopo yote ya miaka ya nyuma iliyotolewa kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu.
- Itatunga Sheria kuhakikisha kuwa Mikopo ya Elimu ya juu itakuwa ni kwa ajili ya gharama za kujikimu tu (Meals & Accomodations).
- Itafuta mikopo yote ya wahitimu wote watakaoingia mikataba maalum na Serikali ya kufanya kazi kwa miaka mitatu mfululizo katika maeneo ya pembezoni na yenye mazingira magumu ya kazi, kwa zile sekta mahsusi.

- Italipa Ada ya Masomo, Fedha za Vitabu, na gharama za Mafunzo kwa Vitendo kwa kila mwanafunzi anayedahiliwa kwenye Chuo Kikuu.




- Itarasimisha na kulipia mafunzo kwa vitendo, kwa fani zote kwa kipindi kisichopungua miezi sita ili wanafunzi wote wapitie mafunzo kwa vitendo kikamilifu, vilevile kuweka utaratibu wa kutumia matokeo ya mafunzo kwa vitendo katika utoaji ajira ili kuhimiza wanafunzi kuona umuhimu wa mafunzo kwa vitendo.
- Itaweka vivutio maalum vya kikodi kwa makampuni binafsi yatakayotoa nafasi kwa vijana waliohitimu kufanya mafunzo kwa vitendo.
- Itahakikisha vyuo vikuu vyote nchini vinaweka sheria kali na taratibu mahususi kuzuia rushwa ya ngono.

**b). Namna gani tutaimarisha huduma za Afya?**

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itasimamia ujenzi wa zahanati mijini na vijijini kufikia lengo la kuwa na zahanati 1 kwa watu 1000.




- Itajenga na kuboresha hospitali za mikoa na kuzifanya ziwe za kisasa na zenye kukidhi viwango vya kimataifa, ikiwa ni pamoja na kuwekeza na kuboresha huduma za uchunguzi kwenye kila hospitali ya mkoa.
- Itafanya uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya afya kwa kuwa na hospitali kubwa tatu za kanda zenye hadhi, uwezo na viwango vya kimataifa. Hospitali hizo zitajengwa katika mikoa ya Mara, Ruvuma na Singida.
- Itawekeza kwenye mfumo wa TEHAMA utakaoweza kukusanya na kuhifadhi taarifa za wagonjwa nchi nzima kwa urahisi, ufanisi, uhakika na kwa wakati, hivyo kuwafanya matabibu kuwa na historia sahihi ya mgonjwa.

**Tutawajali zaidi Wafanyakazi wa sekta ya afya**

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

- Itasimamia utaratibu wa wanafunzi wa shahada ya kwanza ya utabibu, kupewa mafunzo ya huduma za afya ya msingi kama sehemu ya mafunzo kwa vitendo (internship), kabla ya kuhitimu masomo yao.
- Itatenga fedha maalumu za ufadhili kwa masomo ya utabibu na ukunga ili kufikia lengo la kuwa na daktari mmoja kwa kila watu 1,000 ifikapo mwaka 2030.

**Na kuhusu utoaji wa huduma je?**

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

- Itahakikisha katika kila nyumba 100 kunakuwa na mtaalamu wa afya (bibi/bwana afya), ili kufuatilia mienendo ya afya za Wananchi kwa kuangalia historia za afya ya familia, hali ya mazingira, usafi wa nyumba nk.
- Msisitizo mkubwa utawekwa kwenye 'elimu ya kinga' kabla ya 'tiba'.
- Kuhakikisha wazee, mama wajawazito, watu wenye ulemavu ambao wanahitaji huduma za afya mara kwa mara, pamoja na wanawake, na watoto wahanga wa ukatili watapatiwa matibabu bila malipo.
- Kuhakikisha kila hospitali ya wilaya inakuwa na daktari bingwa wa akina mama na watoto.
- Kutoa bure chanjo za magonjwa mbali mbali, hasa kwa ajili ya watoto na zenye kulinda watanzania juu ya magonjwa yenye kuambukiza ay a milipuko.
- Itaboresha mfuko wa Bima ya Afya kwa kuunganisha na mifumo ya Hifadhi ya Jamii, ili kila Mtanzania anapochangia hifadhi ya jamii awe anapata huduma ya Afya moja kwa moja.
- Itaisimamia kikamilifu haki ya kila Mtanzania kuwa na Bima ya Afya yenye kumpa kinga ya matibabu bila kujali hali yake ya kiafya (wakati wa kujiunga na bima).

**Tutahakikisha Dawa na vifaa vya matibabu vinapatikana**

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itawekeza kwenye utafiti na uzalishaji wa dawa salama ndani ya nchi pamoja na vifaa tiba.
- Itaweka utaratibu maalumu wa kuwezesha kimitaji viwanda vya ndani na vyuo vya ufundi ili viweze kuzalisha dawa na vifaa vya tiba kwa kiwango cha kimataifa, ili kukidhi soko la ndani na kushindana katika soko la nje.
- Itaimarisha mfumo wa usambazaji dawa na vifaa tiba kwa kutumia teknolojia mbalimbali za mawasiliano, na kudhibiti ubora wa dawa na vifaa vya afya vinavyotumika nchini.



**c). Tunaahidi nini kuhusu huduma ya Maji?**

Ili kuhakikisha upatikaji wa maji safi na salama kwa kila Mtanzania, Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itawekeza wastani wa Shilingi Trilioni 2 kwa kila mwaka, kwenye kumaliza kabisa tatizo la maji safi na salama kwa Wananchi. Hii ni pamoja na kujenga na kupanua miundombinu ya maji safi na maji taka.
- Itaimarisha Mfuko wa Maji kwa kuupa chanzo cha uhakika cha mapato kutoka Ushuru maalumu utakaotokana na matumizi ya mafuta ya Petroli nchini.
- Itatoa ruzuku kwa Mamlaka za maji ili kuziwezesha kupanua na kuboresha miundombinu ya maji katika maeneo yao. Upanuzi wa miundombinu ya maji utazingatia mahitaji, usawa na mipango ya miji/vijiji na si nani anaweza kulipa ankara, shabaha ni kuyafanya maji kuwa huduma ya muhimu na sio biashara.



- Itatoa ruzuku ya upatikaji wa maji bure kwa kaya masikini, zinazoendeshwa na wanawake au kaya zinazoishi na watoto wenye ulemavu wanaohitaji uangalizi maalum.
- Itaratibu huduma za maji zinazotolewa na watu binafsi ili kudhibiti usalama wa maji na gharama za huduma hiyo.
- Itawekeza katika kuhamasisha vijana kuvumbua mbinu mbalimbali za kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama, uhifadhi endelevu wa maji safi hasa ya mvua na udhibiti wa maji machafu nchi nzima.

### d). Tutahakikishaje Nishati endelevu?

Bila kuwa na nishati endelevu, inayopatikana kwa uhakika muda wote, hakutakuwa na ufanisi katika viwanda, ubunifu na utoaji wa huduma bora za jamii. Hivyo, tutafanya yafuatayo:

- Itaongeza matumizi ya gesi ya Mtwara kuzalisha Umeme kutoka chini ya 20% hadi 60% kufikia mwaka 2025, kwa kujenga vituo vya kuzalisha umeme katika Mikoa ya Mtwara na Lindi na kuingiza umeme huo kwenye Gridi ya Taifa.
- Itaongeza kiasi cha umeme kinachozalishwa kutoka megawati 1,500 za sasa mpaka megawati 5,400 kufikia mwaka 2025 kutokana na vyanzo mbalimbali vya nishati jadidifu ikijumuisha umeme jua, makaa ya mawe, upepo na joto ardhi.
- Itatumia nishati ya umeme jua inayopatikana bure kuhudumia zahanati, vituo vya afya, shule za msingi na sekondari za Serikali ili kupunguza mzigo kwenye gridi ya taifa, kuondoa gharama za usafirishaji na usambazaji wa umeme kwenye taasisi hizo nchi nzima na kuwa na umeme wa uhakika unaozalishwa kwenye kila taasisi.
- Itasambaza bomba la gesi majumbani kwa matumizi ya kupikia ili kupunguza gharama za kutumia umeme, kununua mitungi ya gesi na kuokoa mamilioni ya misitu inayopotea kila mwaka kwa matumizi ya kupikia majumbani.
- Itaendelea kusambaza umeme kwa kasi hasa vijijini, sambamba na kupunguza gharama za umeme. Kuunganisha mikoa na wilaya zote kwenye grid ya taifa.

- Itapunguza gharama za umeme kwenye matumizi ya kijamii, kama gharama za kusukuma maji, ili kupunguza gharama za kulipia maji kwa wananchi.




## e). Tumekusudia nini kuhusu Hifadhi ya Jamii?

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itawezesha kila Mtanzania kujiunga na mfumo wa hifadhi ya jamii. Mifuko ya hifadhi ya jamii itaunganishwa moja kwa moja na huduma za afya na bima ya majanga ili kupunguza msururu wa michango/mifumo hasa kwa Watanzania walio katika sekta binafsi na kwa waajiri.
- Itapunguza michango kwenye hifadhi ya jamii kutoka asilimia ishirini (20%) ya sasa mpaka asilimia kumi na mbili (12%), kwa mchanganuo wa asilimia tisa (9%) kuwa mchango wa akiba ya hifadhi ya jamii, asilimia mbili (2%) kuwa mchango wa Bima ya Afya, na asilimia moja (1%) kuwa mchango wa mfuko wa fidia kwa wafanyakazi (WCF),

- Itashirikiana na na wataalamu wa huduma za fedha ili kutengeneza mfumo wa bima ya majanga utakaowalinda wananchi hasa wa hali ya chini, wafanyabishara wadogo na wakulima dhidi ya majanga yanayotokana na milipuko ya magonjwa, mafuriko, matetemeko, moto, n.k.
- Italeta fao la bei kwa mazao ya kilimo kwa wakulima wote watakaokuwa wanachama wa mpango wa Hifadhi ya Jamii.
- Itatumia Mpango wa Hifadhi ya Jamii kwa wakulima kuendesha miradi mikubwa ya kimkakati ya kuleta mapinduzi ya Kilimo nchini, hasa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, maghala ya uhifadhi na viwanda vya usindikaji.

f). Jinsi gani tutahakikisha Makazi Bora?

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itawekeza kwenye teknolojia itakayosaidia ufanisi wa kupanga miji. Ndani ya miaka mitano, Serikali yetu itakamilisha upimaji wa miji nchi nzima ili kuhakikisha wananchi wanaishi kwenye maeneo yaliyopimwa na yenye huduma muhimu za jamii.
- Itaweka utaratibu, kushirikiana na sekta binafsi, hasa taasisi za kifedha, kuwezesha vikundi/ushirika wa vijana mafundi wa nyumba/makazi ili kukuza na kuboresha ufanisi wa sekta ya ujenzi wa makazi nafuu.
- Itaanzisha utaratibu maalumu wa kuboresha makazi holela hasa kwenye maeneo ya miji, na kufanya kila Mtanzania kuishi kwenye makazi yaliyo salama, ya kiutu, yanayofikika na yenye huduma zote muhimu za jamii.
- Itaratibu sekta ya upangishaji na ununuzi wa nyumba ili iweze kunufaisha Watanzania wote hasa wa hali ya chini.



## JE, TUNA MIKAKATI GANI YA KUKUZA UCHUMI WA WATU?

Ili nchi iwe na uchumi imara na endelevu ni lazima wananchi wake wamiliki uchumi kupitia biashara, kilimo, huduma, uvuvi, ufugaji, utalii n.k. Katika kuhakikisha kwamba uchumi wa watu unaimarika na Serikali inapata mapato yake, Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

a). Tutaboresha mazingira ya Biashara

- Itawapa wananchi uhuru na kuondoa urasimu katika kuanzisha na kuendesha biashara yoyote ikiwa ni pamoja na uhuru wa kununua na kuuza bidhaa zozote halali ndani na nje ya nchi bila vikwazo vyovyote.
- Itaunda mfuko maalumu wa kutoa udhamini, ufadhili na mikopo kwa biashara zinazochipukia zenye ubunifu, hasa ambazo zimejikita katika matumizi ya teknolojia na zinazomilikiwa na vijana na wanawake.



- Itazitambua na kurasimisha biashara zilizo nje ya mfumo rasmi ili kuzipa uwezo na fursa ya kupata mitaji, teknolojia na masoko.
- Itatambua na kuweka mazingira mazuri ya kisera ili kuendesha biashara kwa njia ya mitandao kwa mafanikio makubwa hasa kwa Watanzania.
- Itawalinda wafanyabiashara na wazalishaji wa ndani na kuwajengea mazingira ya kushirikiana na/au kushindana na wafanyabiashara na bidhaa kutoka nje ya nchi.
- Serikali ya ACT Wazalendo itaondoa mfumo unaomlazimisha mfanyabiashara kulipa kodi kabla hajaanza kufanya biashara.




- Itatumia ofisi zake za kibalozi duniani kote kutafuta na kuwezesha upatikanaji wa fursa za kibiashara na washirika wa kibiashara nje ya nchi, ili kuimarisha urari wa kibiashara, kuongeza fedha za kigeni hapa nchini na kuitangaza Tanzania kama mzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

- Itahamasisha na kuwawezesha wawekezaji wa ndani katika sekta ya viwanda, uzalishaji na umiliki wa miundombinu kama vile umeme, maji, ndege, nishati ya gesi, vivuko n.k., kupitia mfumo wa Ubia wa Sekta binafsi na Sekta ya Umma.
- Itawauzia Watanzania mpaka asilimia 51 za hisa za makampuni makubwa yanayomilikwa na Serikali kwa sasa ili wananchi washiriki moja kwa moja kumiliki uchumi wao na kuongeza ufanisi na uwazi wa mashirika hayo kupitia masoko ya mitaji.
- Itapitia mifumo yote ya kodi na kuhakisha kunakuwa na kodi rafiki kwa wananchi. Kodi sahihi zinazotozwa kwa wakati sahihi ili kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiyari, na muhimu zaidi ili kuhakisha biashara zinakua na kuimarika na siyo kuwa na mfumo wa kodi ambao utapelekea kufunga au kuua biashara.

**b). Uhakika wa Ajira zenye maslahi**

- Serikali yetu itatengeneza ajira zenye tija milioni kumi (10) ndani ya miaka mitano. Ajira milioni tano (5) kutoka kwenye mnyororo wa thamani wa sekta ya kilimo, ajira milioni 2 kutoka sekta rasmi na ajira milioni 3 kutoka sekta isiyo rasmi.
- Itaweka mifumo mizuri ya kisera na uwekezaji katika soko la sanaa na michezo, Serikali yetu kupitia wizara husika itafanya uwekezaji wa kina kwenye kuimarisha, kuinua na kutengeneza ajira zenye tija zisizopungua laki tano kwenye soko la sanaa na buruduni na mnyororo wake wa thamani.
- Itaimarisha ubora na kutafuta soko la nje kwa kazi za ubunifu kama uhunzi, uchongaji, uchoraji na bidhaa zingine zitokanazo na kazi za mikono.
- Itaboresha maslahi ya wafanyakazi wa sekta ya umma na kusimamia maslahi stahiki ya wafanyakazi wa sekta binafsi ili ajira zote zitakazozalishwa kipindi cha uongozi wetu ziwe ajira zenye tija na zenye kukidhi mahitaji ya wafanyakazi na kupatiwa hifadhi ya jamii stahiki.

- Itapunguza kodi ya wafanyakazi (PAYE), lengo likiwa kuwaongezea wafanyakazi kipato ili waweze kumudu mahitaji katika maisha, kujiwekea akiba au kuanzisha na kuendesha shughuli za uzalishaji kipato cha ziada.
- Itatengeneza mazingira mazuri ya kisera yatakayowezesha vyama vya wafanyakazi kuwa huru, kuimarika na kusimamia maslahi ya wafanyakazi kwa ufanisi.
- Kulipa mafao ya watumishi kwa wakati na kuboresha maslahi na huduma kwa wastaafu.

**c). Tutawezekeza zaidi sekta ya Michezo, Sanaa na Burudani**

Tanzania imejaaliwa vibaji na vipawa vya hali ya juu katika nyanja ya sanaa na michezo. Ili kufufua utajiri uliojificha kwenye sekta hiyo, Serikali yetu itafanya yafuatayo:

- Kurudisha Serikalini maeneo ya wazi yaliyoporwa, na kutenga maeneo mapya ya wazi kwa ajili ya michezo na mapumziko. Serikali yetu itaingia ubia na vikundi vya wanawake na vijana katika kuhakikisha maeneo ya wazi yanatumika kwa ajili ya burudani, starehe pamoja na kutengeneza ajira kwa vijana.
- Kuunda Mamlaka ya Viwanja vya Michezo ili kujenga, kuendeleza na kutunza Viwanja vya michezo kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi.
- Kutengeneza Sera ya Mambo ya Nje ambayo, michezo na burudani ni moja kipaumbele cha mashirikiano yetu na nchi nyingine.
- Kujenga kumbi tano kubwa za matamasha Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma ili kuhakikisha sanaa inapewa hadhi na thamani yake na Watanzania wanakula bata kwenye mazingira mazuri.
- Kutoa ruzuku ya Kikodi kwa Kampuni Binafsi au watu binafsi wanaowekeza kwenye sekta ya michezo. Kwa mfano Kampuni binafsi yenye timu za michezo, kama mpira wa miguu, mpira wa meza, mpira wa mikono nk. kuruhusiwa kuondoa gharama za uendeshaji wa Timu katika kukokotoa kodi ya Mapato.

- Kuwezesha uwekezaji kwenye shule za michezo kwenye Kanda zote 8 za nchi yetu ikiwemo kuhamasisha mashirika ya umma kuanzisha, kumiliki na kuendesha timu za michezo mbalimbali pamoja na Shule za Michezo ili kukuza michezo nchini na kukuza vipaji vya Vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

**d). Tutakuza Kilimo, mifugo na uvuvi**

Katika kuhakikisha kwamba tunapata mapinduzi makubwa, Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itatenga 20% ya bajeti ya maendeleo kwenye Sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi, mara mbili zaidi ya makubaliano yaliyozimiwa na Umoja wa Afrika.
- Itapanua na kuboresha vyuo vya kilimo, na kuwekeza kiasi kisichopungua shilingi bilioni 100 kwa mwaka katika utafiti, usambazaji wa mbegu bora za kilimo na kutengeneza mnyororo wa thamani kwa kila zao linalozalishwa hapa nchini.
- Itafungamanisha sekta ya kilimo na sekta ya viwanda, kwa kuhakikisha kwamba viwanda vya ndani vinapata zaidi ya asilimia 80 ya mahitaji yao kutoka kwa wakulima, na kwamba wakulima wanafaidi bei nzuri ya mazao yao na soko la uhakika.
- Itabainisha aina ya mazao ya kimkakati kwa kila mkoa/kanda na kuhamasisha uzalishwaji wake kwa wingi, ikiwa ni pamoja na kuweka mpango mzuri wa kuongeza thamani ya mazao hayo kabla ya kuyauza kwenye masoko ya ndani na nje.
- Itaruhusu wakulima, wavuvi na wafugaji kuuza mazao yao popote watakapo ndani na nje ya nchi bila vikwazo au masharti magumu.
- Itaanzisha mfuko maalumu wa kilimo kwa ajili ya kutoa ruzuku kwa miradi ya kimkakati ya kilimo, hasa miradi ya uanzishwaji wa viwanda vya kusindika na kusambaza mazao ya wakulima.
- Itapanua huduma za Benki ya Kilimo kila mkoa. Tutaimarisha na kuiongezea uwezo ili iweze kutoa mikopo yenye riba ndogo na inayolipwa kulingana na msimu wa kilimo.

- Itaondoa unyonyaji unaofanywa na madalali kwenye soko la mazao, kwa kuimarisha mfumo wa taarifa ya masoko ya mazao, kwa kutumia mifumo ya TEHAMA itakayowezesha wakulima kuuza mazao yao moja kwa moja kwa mtumiaji kwa njia ya mtandao.




- Itatoa msukumo wa pekee kwa mazao ya michikichi, alizeti na miwa, ikiwa ni pamoja na kuchochea uanzishaji wa viwanda vingi vya kuzalisha mafuta ya kula na sukari ili ndani ya miaka 5 tuache kabisa kuagiza mafuta na sukari kutoka nje ya nchi.
- Itawekeza katika miundombinu ya umwagiliaji inayolinda na kuhifadhi mazingira. Msukumo mkubwa utawekwa kwenye umwagiliaji endelevu kwa kutumia nishati ya jua ili kuwaendeleza wakulima wadogo na wakati kutumia maji yaliyo chini ya ardhi.
- Itawekeza katika uhifadhi, uzalishaji na usambazaji wa mbegu asilia, ama ziwe za jadi au zilizoboreshwa na kukomesha matumizi ya mbegu zilizobadilishwa vinasaba maabara.

- Itatoa kipaumbele maalumu kwenye kilimo cha mbogamboga na matunda, hasa kwa uwezo wake wa kuingiza fedha za kigeni kutokana na ukubwa wa soko la kigeni, lakini pia ni kilimo kinachofanywa zaidi na wanawake na vijana, hivyo kutengeneza ajira kwa makundi hayo.
- Itajenga maghala kwa ajili ya kuhifadhi nafaka, na majokofu kwa ajili ya kuhifadhi mbogamboga na matunda, katika kila wilaya ya Tanzania bara na mikoa yote Tanzania visiwani.
- Katika kutambua mchango wa uvuvi na ufugaji, itawekeza na kuhakikisha uvuvi na ufugaji endelevu unafanyika kote nchini, ikiwemo kuwekeza katika minada ya kisasa na kupanua soko la bidhaa za ufugaji na uvuvi ndani na nje ya nchi.

**e). Tutafanya nini kuboresha matumizi ya Ardhi?**

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itaanzisha mfumo mpya unaozingatia ushirikishwaji wa wananchi kutoka katika ngazi za utumiaji, umiliki na usimamizi/udhibiti wa ardhi kupitia vyombo vya uwakilishi vilivyo karibu na wananchi.
- Itaweka utaratibu wa kuzijengea uwezo halmashauri za vijiji, kamati za ardhi za vijiji na mabaraza ya ardhi ya vijiji katika kusimamia ardhi na utajiri wote uliopo ndani ya mipaka ya vijiji kwa niaba ya umma wa vijiji husika.
- Itazilinda kisheria na kuzipa hadhi sawa haki za umiliki wa ardhi ya kimila kama ilivyo kwa hati zinazotolewa na serikali kuu.
- Itaondoa utaratibu wa kutoza kodi za ardhi kwa ardhi za kijiji, kutokana na ukweli kwamba dhana ya umiliki kati ya wanakijiji hutofautiana na ile ya wawekezaji ambao hutumia ardhi kwa ajili ya kuzalisha faida au kulimbikiza mali wakati wananchi, wakulima wadogo hutumia kujikimu na kujihifadhi.

- Itafuta gharama za upimaji wa viwanja nchi nzima, kupanga miji ni utakuwa wajibu wa Serikali yetu.




- Itarejesha na/au kugawa upya ardhi kwa Wananchi walioporwa na walionyang'anywa kupitia ubinafsishwaji kutoka kwa mashiriki ya Umma na makampuni hodhi.
- Ili kuondoa ukiritimba wa umilikaji wa ardhi, itaunda baraza la Ardhi la Taifa kama chombo huru kitakachokuwa na miliki ya hati ya ardhi ya jumla na ardhi ya hifadhi, ambalo litawajibika kwa chombo chenye uwakilishi wa wananchi kitaifa (bunge).

**f). Tumekusudia kufanya nini kuhusu Miundombinu?**

Tunaamini miundombinu bora, yenye kufikia wengi na kurahisisha ufanyaji kazi na ufanisi ni nguzo ya uchumi wa watu. Hivyo, Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itaendeleza juhudi za kufufua reli ya kati na kuunganisha mikoa kwenye mfumo madhubuti wa reli utakaorahisisha usafirishaji wa bidhaa kwa urahisi ndani na nje ya nchi.

- Itajenga reli ya kuunganisha mradi wa Mchuchuma na Liganga na Bandari ya Mtwara ili kusafirisha madini ya chuma, bidhaa za chuma, makaa ya mawe na bidhaa nyengine zinazotokana na mradi huo.
- Itajenga reli ya kuunganisha mradi wa Kabanga Nickel na reli ya kati ili kusafirisha madini ya Nickel kupitia bandari za Dar na Bagamoyo.
- Itajenga mifumo imara ya barabara hasa kutoka kwenye vijiji na mashamba ya ushirika ya wakulima wadogowadogo na kuunganisha na barabara kuu.
- Itajenga barabara kwenye maeneo yanayozalisha mazao makuu yanayoliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni. Katika miaka mitano inayokuja tutajenga barabara ya korosho kwa kutumia fedha zinazotokana na ushuru wa korosho.
- Itajenga masoko ya kisasa kila wilaya, na kuhakikisha masoko yote makubwa na madogo, yana mifumo sahihi ya ukusanyaji na uteketezaji taka, maji safi, mifumo ya maji taka, mahali stahiki kwa uhifadhi wa bidhaa mbalimbali na vyoo vya kutosha.
- Itahakikisha vyoo vya umma vinajengwa katika kila maeneo ya wazi yenye mikusanyiko ya watu nchi nzima.

**g). Tutaimarishaje Viwanda vyetu?**

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

- Itawezesha uwekezaji kwenye viwanda vinavyozalisha vifaa mbalimbali vya viwandani au bidhaa/machine zinazotumika kutengenezea bidhaa nyingine kwa kuweka vivutio stahiki.
- Tutahakikisha kuwa hatutaendelei kuwa soko la teknolojia inayozalishwa na nchi nyingine, bali na sisi tunakuwa wazalishaji wa teknolojia mbalimbali hasa teknolojia za kukabiliana na changamoto zetu watanzania na wa Afrika. Viwanda hivi kwa teknolojia vinatarajiwa kuajiri vijana wasiopungua laki tano kwenye mnyororo wake wa thamani.




- Itawezesha ufufuaji wa viwanda vya kuchakata pamba na kuzalisha nguo ili kuzalisha bidhaa kama vitenge, vijora, madera na batiki zenye ubora wa hali ya juu.
- Itaboresha vivutio ili kuwezesha ujenzi wa viwanda vidogo maeneo ya vijijini vinavyoendeshwa, kumilikiwa na kusimamiwa na wakulima wenyewe kupitia vyama vyao vyao vya ushirika, ambavyo vitaweza kuzalisha ajira na kuchakata mazao.
- Itawezesha uwekezaji kwenye viwanda vya kusindika matunda, nyama, samaki na mbogamboga na kuongeza thamani badala ya kuuza mazao kama yalivyotoka shambani.




**h). Tutafanya nini kuwezesha nchi yetu ifaidi Utajiri wa maliasili?**

Tanzania imebahatika kuwa na maliasili nyingi ambazo ni utajiri mkubwa ikiwa zitatumika vyema. Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

- Itarekebisha sera za kodi ili kuirejesha katika hali yake ya kawaida sekta ya Utalii pamoja na mnyororo wake ambayo imeathirika sana na janga la Virusi vya Corona. Marekebisho hayo yatahusisha kutoa ruzuku kwa Kampuni za Utalii na kulinda Ajira za Wafanyakazi wa Sekta ya Utalii.
- Itawekeza kwenye Ujenzi wa miundombinu ya Maeneo ya Utalii ili kufungua vivutio vipya na kuvifanya kufikika kwa urahisi na kwa usalama.
- Itawezesha Sekta Binafsi kuongeza vyumba vya mahoteli kwenye vivutio vya Utalii,
- Itaanzisha kampeni Maalumu ya kufikisha Idadi ya Watalii Milioni 5 watakaoingia nchini ifikapo Mwaka 2025.
- Itatumia sekta ndogo za Michezo na Burudani kimkakati kama nyenzo za kukuza Utalii nchini.

### i). Vipi kuhusu Bahari na Bandari zetu?

Serikali yetu itatumia nafasi ya Tanzania kijiografia, ya kuzungukwa na nchi nyingi zisizo na bahari, kufaidika kiuchumi kwa kuifanya Tanzania kuwa kituo kikuu cha usafirishaji wa majini na kitovu kikuu cha biashara eneo la Maziwa Makuu. Kufikia shabaha hii, Serikali ya ACT Wazalendo itahakikisha yafuatayo:

- Kufufua na kuendeleza uwekezaji wa eneo la kiuchumi la Bagamoyo.
- Kuimarisha Bandari ya Mtwara ili kuhudumia korido ya maendeleo ya Mtwara ambayo inahusisha mradi wa Mchuchuma na Liganga na Usafirishaji wa Bidhaa kutoka na kwenda katika nchi ya Malawi na kaskazini mwa nchi ya Msumbiji. Vilevile, kuufanya Mji wa Mtwara kuwa kituo cha huduma kwa miradi ya uwekezaji wa mafuta na gesi, kusini mwa Tanzania na Kaskazini mwa Msumbiji.
- Kuimarisha Bandari ya Tanga, kwa kukamilisha uwekezaji wa Bandari ya Mwambani.
- Kuimarisha Bandari ya Kigoma ili kuweza kuhudumia mizigo inayotoka na kwenda mashariki ya Kongo pamoja na nchi ya Burundi.
- Kuwezesha uwekezaji kwenye bandari za uvuvi ili kuimarisha uvuvi bahari kuu kufikia lengo la mauzo nje ya mapato ya uvuvi yenye thamani ya dola za kimarekani bilioni 1.

### j). Sekta ya madini Madini je?

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya mapinduzi makubwa katika mfumo wa umiliki na uendeshaji wa miradi katika sekta ya uchimbaji wa madini ili kuhakikisha wananchi wanafaidika na rasilimali hii. Ili kutekeleza hilo, Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

- Itabadili mfumo wa umiliki ili uwekezaji kwenye madini kuwa ni kwa utaratibu wa kugawana mapato kati ya mmiliki na Mwendeshaji.
- Itaweka mkazo kwenye miradi ya uchimbaji madini ambayo ina faida kubwa ya fungamanisho, miradi mikubwa miwili ya

kipaumbele itakuwa ni Mradi wa Mchuchuma na Liganga wilayani Ludewa, mkoani Njombe, na mradi wa Kabanga Nickel wilayani Ngara, mkoani Kagera.

- Itaweka kisheria utaratibu wa wananchi wanaoishi kwenye maeneo yenye madini kutoa idhini ya mradi wa uchimbaji madini kabla ya kuanza kutekelezwa.




## k). Tutalindaje Mazingira?

Mazingira ndiyo uhai wa taifa hili. Hivyo, Serikali ya ACT Wazalendo itahakikisha kuwa;

- Shughuli zote za maendeleo zinaheshimu, kuhifadhi na kulinda mazingira.
- Inaheshimu mikataba yote ya kimataifa ya kulinda mazingira ikiwemo Mkataba wa Makubaliano ya Uhifadi Mazingira ya Paris.

- Inapunguza hewa ya ukaa na matumizi ya plastiki.
- Inawezesha NEMC kuwa shombo kinachofanya kazi kwa karibu na idara zote muhimu za Serikali.
- Makampuni na viwanda vikubwa wanachangia mfuko wa ruzuku wa miradi ya kulinda mazingira.
- Elimu ya asili ya utunzaji mazingira, inahifadhiwa na kutumika katika shughuli mbali mbali za kutunza mazingira.



## JE, MIRADI GANI YA KIMKAKATI TUMEIKUSUDIA?

Serikali ya ACT Wazalendo itatekeleza miradi ifuatayo ya kimkakati;

- Itasimamia kukamilika kwa uwekezaji wa mradi wa Mchuchuma na Liganga kuzalisha bidhaa za chuma, madini ya vanadium na madini mengine, umeme wa makaa ya mawe na kuongeza mapato ya fedha za kigeni.
- Itasimamia Ujenzi wa mabwawa makubwa 5 ya kuzuia mafuriko na kujenga skimu kubwa za umwagiliaji zenye jumla ya hekta 1,000,000.
- Itatekeleza Ujenzi wa miradi ya maji nchi nzima kuhakikisha kila mtanzania anapata maji safi na salama kutoka mapato ya ushuru wa mafuta ili kumaliza kabisa tatizo la maji safi na salama.
- Itawezesha Ujenzi wa barabara ya Korosho [Nangurukuru – Liwale – Nachingwea – Masasi – Newala – Tandahimba – Mtwara – Lindi – Nangurukuru] kutokana na mapato ya ushuru wa korosho ili kufungua wilaya zinazolima korosho na kufungua Wilaya ya Liwale kwa kufungua barabara za Songea-Liwale na Liwale-Morogoro.
- Itasimamia uwekezaji wa eneo maalumu la kiuchumi la Bagamoyo ili kuifanya Tanzania kuwa kituo cha usafirishaji wa majini katika Afrika na eneo la maziwa makuu na kuongeza ajira na mapato ya fedha za kigeni.
- Itasimamia kukamilika kwa Uwekezaji wa kinu cha kuchakata gesi asilia (LNG) ili kuongeza mapato ya fedha za kigeni, ajira na maendeleo ya viwanda nchini.
- Itasimamia kukamilika kwa Uwekezaji wa mradi wa uchimbaji madini ya Nikeli katika eneo la Kabanga, wilayani Ngara, mkoani Kagera.

- Itafanya uchambuzi wa kina kwa miradi inayoendelea sasa, kama vile mradi wa Reli ya Kati (SGR), Mradi wa Umeme wa Maji Mto Rufiji (Stiglers Gorge), na Ufufuaji wa Shirika la Ndege la Taifa (ATCL). Lengo la uchambuzi huu ni kuiondoa Serikali kwenye angalau 50% ya gharama za utekelezaji ili kuelekeza rasilimali fedha kwenye miradi ya huduma za jamii, kama elimu, maji na afya, na kwenye miradi itakayochochea maendeleo ya watu, kama kilimo cha umwagiliaji.





## JE WAJUA NCHI YETU ITAKUWA YA NAMNA GANI MWAKA 2025?

Ifikapo mwaka 2025 Tanzania itakuwa na jumla ya watu milioni 71. Serikali yetu itakuwa inakabiliana na jukumu la kuongeza shughuli za kiuchumi ili kukidhi haja ya ongezeko la watu, vijana wanaotaka ajira nyingi na huduma muhimu kama Elimu na Afya.

- Baada ya miaka mitano ya Uongozi wa Serikali ya ACT Wazalendo, na utekelezaji wa Sera zetu, tunataka Taifa letu liwe na matokeo yanayotupelekea kwenye uchumi unaokua, uliochangamka na jumuifu ambapo;
- Wastani wa pato la mtu mmoja litakuwa Dola za Marekani 1,300.
- Watanzania wanaoishi chini ya mstari wa umasikini kuwa 14% tu,
- Ukosefu wa ajira kuwa chini ya 8%, na
- Asilimia 60 ya watu wote wanaojihusisha na shughuli za kilimo, uvuvi, ufugaji na biashara ndogo zilizosajiliwa wamekuwa na Hifadhi ya Jamii na wananchi wote kuwa na Bima ya Afya.
- Haya yatakuwa ni matokeo ya Sera na mikakati ambayo katika miaka mitano (2020-2025) itafanikisha;
- Uwekezaji katika uchumi wa vijijini, kupitia ushirika wa kisasa ambao utawezesha mapinduzi ya kilimo na kuongeza thamani mazao ya kilimo na hivyo kuwezesha sekta ya kilimo kukua kwa kasi ya 8-10% kwa mwaka kuanzia mwaka 2022.
- Uwekezaji kutoka nje katika sekta zote za uchumi na kuifanya Tanzania kuwa nchi inayoongoza kupokea uwekezaji  katika eneo la Maziwa Makuu.
- Uwekezaji katika elimu ya msingi, elimu ya ufundi na asilimia 50 ya Mikoa ya Tanzania Bara kuwa na chuo cha ufundi na elimu ya juu kwa kuwa na vyuo vikuu vipya vya Taifa vitano vyenye wanafunzi 20,000 kila kimoja.

- Uwekezaji katika afya kwa kuwa na hospitali kubwa 3 za Kanda; katika kanda ya ziwa, Nyanda za juu kusini na Kanda ya kati zenye uwezo, ukubwa na viwango vya kimataifa kwenye kutoa huduma.
- Uboreshaji wa muundo wa Muungano kufuatia kupitishwa kwa Katiba mpya: Muungano wa Serikali Tatu na wenye Usawa, Haki na wa kuheshimiana.
- Serikali za Mitaa kuwa na uhuru wa kupanga maendeleo ya watu wao na kuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato.
- Kuwa na Serikali za Mikoa ambazo wananchi wanawachagua wakuu wa mikoa kuanzia uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.



ACT WAZALENDO

# SAFARI YA KUREJESHA FURAHA IMEANZA. KARIBU NAWE USHIRIKI.

Kazi tuliyonayo si ya mtu au kikundi kimoja. Ni jukumu letu sote. Sio suala la utajiri au kipato kikubwa. Ni suala la moyo wenye matumaini ya kurejesha raha na ndoto zilizovunjika. Kwa moyo na ushirika mmoja - **WOTE TUNAWEZA.**

NMB Close to you

## NMB (T) Ltd

Mikocheni Branch

A/c Name: **ACT WAZALENDO UCHAGUZI**

A/c Number: **22610026136**

Swift Code: **NMIBTZTZ**

m-pesa

## Mpesa

A/c Name: **ACT Wazalendo**

PhoneNumber: **+255 744 959112**

## Kupitia Tovuti

www.actwazalendo.or.tz/donation_options

P.O. Box 105043, Dar es salaam | info@actwazalendo.or.tz
www.actwazlendo.or.tz | +255 712 622642 / 653 619906